# FORM FOUR TERM ONE EXAM 2017

**WONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/1**

**Majibu ya ufahamu**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/1

1. (a) Sura ya ripoti ihusu:
   (i) Anwani ya ripoti ionyeshe yahusu nini.
   (ii) Utangulizi.
      - Wanajopo wenyewe.
      - Kazi waliyopewa.
      - Aliyeliteua jopo.
      - Muda wa kuwasilisha kazi.
   (iii) Utaratibu wa kufanya utafiti/njia za kukusanya data.

   (b) Mwili/matokeo ya uchunguzi wenyewe/hoja zenyewe/maudhui.
   - Kuwepo kwa silaha haramu.
   - Viongozi kuwachochea raia.
   - Kuwepo kwa vikundi haramu
   - Ukosefu wa kazi.
   - Ukosefu wa amani katika nchi jirani.
   - Kutowajibika kwa askari.
   - Umaskini
   - Ufisadi wa raia na mahakama.
   - Ushindani katika biashara.
   - Kuabudu mashetani.
   - Mihadarati.
   - Ugaidi.
   - Sheria duni.
   - Raslimali chache – maji, malisho, chakula n.k. huzua vita.

   (c) Mapendekezo.
   - Wananchi waelimishwe kuhusu madhara ya silaha haramu.
   - Wachochezi wachukuliwe hatua kati.
   - Kupanua nafasi za kazi.
   - Vikundi haramu vichukuliwe hatua za kisheria.
   - Serikali kushirikiana na mataifa mengine kuleta amani katika nchi jirani.
   - Mafunzo yatolewe kwa raia kuhusu maadili n.k.

   (d) Hitimisho.
   - Mwanfunzi atoe mwito.
   - Jina la mwandishi wa ripoti, sahihi na tarehe.

2. Pesa za hazina ya vijana.

   **Faida.**
   - Kuanzisha miradi ya kuwaletea pesa.
   - Kuinua kiwango chao cha maisha.
   - Kuondoa ukosefu wa kazi.
   - Kupunguza uhalifu na kudumisha maadili.
   - Kuwafanya wawajibike maishani.
   - Kuwashirikisha katika ukuaji wa uchumi.
   - Kukuza vipawa vyao.
   - Kuboresha miundo msingi na mazingira kwa jumla.
   - Utangamano wa vijana.

   **Hasara**
   - Ubadhirifu k.m. Kushiriki anasa.
   - Ufisadi miongoni mwa wasimamizi
   - Mapendeleo kinasaba.
   - Chuki na wizi. *(mwanafunzi atoe maoni yake)*

3.Mtahiniwa ahibitishe ukweli wa methali kupitia kisa au visa.
Aonyeshe mhusika anayekosa kuwajibika na anapokosa kufaulu yeye hutoa visingizio visivyo na msingi.

4.Mtahiniwa asimulie kisa kuhusu jumba/jengo lililoporomoka na kuwafunika watu.
Lazima aonyeshe jinsi yeye na wengine walivyojitolea kuwaokoa watu waliokuwa wamekwama kwenye vifusi.
Aonyeshe namna walivyokumbana na tatizo la kuwaokoa mpaka wakashindwa.
Tan. Asiongeze au kupunguza maneno.